

Daudi Atenda kwa Ujasiri

1 SAMWELI SURA YA 17

WAISRAELI WALIKUWA WAKIPIGANA VITA NA WAFILISTI. DAUDI ALIKUWA **MCHUNGAJI**, LAKINI BAADHI YA NDUGU ZAKE WALIKUWA ASKARI-JESHI. HIVYO AKATUMWA KWENDA KUANGALIA HALI YAO.



ASKARI-JESHI WAKAMLETA
DAUDI MBELE YA MFALME
SAULI.

MIMI NITAENDA
KUPIGANA NA
HUYU MFILISTI.

WEWE NI
MVULANA TU.
GOLIATHI AMEKUWA
MWANAMUME WA
VITA KWA MIAKA
MINGI!

LAKINI MIMI
NIMEPIGANA NA
SIMBA NA DUBU
ILI KULINDA
KONDOO WETU.

SAWA.
ASKARI-JESHI,
MVISHENI
MVULANA HUYU
MAVAZI YANGU
YA SILAHA.

SIWEZI
KUTEMBEA NA
MAVAZI HAYA.

MIMI SIHITAJI
MAVAZI YA
SILAHA.


DAUDI AKACHUKUA KOMBEO LAKE, AKAENDA KATIKA BONDE LA MTO, NA KUCHAGUA MAWE MATANO YALIYO LAINI.

YEHOVA
ALINIKOMBOA
KUTOKANA NA
SIMBA NA DUBU.
ATANIKOMBOA
KUTOKA KWA
GOLIATHI.


DAUDI NA GOLIATHI WAKAKUTANA
KATIKA NCHI YA TAMBARARE YA
ELA.

JE, MIMI NI MBWA,
HIVI KWAMBA UNIJIE
NA FIMBO? MVULANA,
NYAMA YAKO
NITAWALISHA NDEGE.

UNAKUJA KWANGU
UKIWA NA UPANGA NA
MKUKI NA FUMO, LAKINI
MIMI NAJA KWAKO NIKIWA
NA JINA LA YEHOVA.



AKIWA NA UHAKIKA KATIKA
YEHOVA, DAUDI **AKAKIMBIA**
HARAKA KUELEKEA KWA
GOLIATHI . . .



NA AKATUPA JIWE, **LIKAMPIGA** GOLIATHI
KATIKA PAJI LA USO WAKE.

JITU HILO LIKAFA, NA HATIMAYE
WAISRAELI **WAKAWASHINDA** WAFILISTI.
MIAKA MINGI BAADAYE, DAUDI AKAWA
MFALME WA ISRAELI.

**TUNAJIFUNZA NINI KUTOKANA
NA HADITHI HII?**

KWA NINI WENGINE **HAWAKUMWAMINI**
DAUDI?

DOKEZO: 1 SAMWELI 17:13, 14,
33, 42.

KWA NINI DAUDI ALIAMINI KWAMBA
ANGEWEZA KUMSHINDA GOLIATHI?

DOKEZO: 1 SAMWELI 16:1, 13; 17:37,
45-47.

KWA NINI **WEWE** UNaweza KUWA NA
UJASIRI WA KUFANYA LILILO SAWA?

DOKEZO: ZABURI 91:11; WAEBRANIA
13:6.